

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA MOJA

02 JUNI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA MOJA – TAREHE 02 JUNI, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

484. MHESHIMIWA JOHN JOHN NCHIMBI (NYASA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Kata ya Mpepo - Nyasa.

485. MHESHIMIWA EDWARD KISAU OLELEKAITA (KITETO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itashughulikia maombi ya kupandishwa hadhi ya Kidato cha Tano na Sita Shule za Sekondari Lesoit, Ndedo, Dongo na Dosidosi.

486. MHESHIMIWA DKT. YAHAYA ESMAIL NAWANDA (NEWALA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Barabara ya Mkoma 1 – Mnyambe – Miyuyu itajengwa.

**487. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE
(LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara za TARURA kwa kiwango cha lami katika Jimbo la Lupembe.

OFISI YA RAIS (MAENDELEO YA VIJANA):

488. MHESHIMIWA AMINA ALI MZEE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Maendeleo ya Vijana):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuendelea kuboresha mafunzo ya ubunifu kwa Vijana nchini.

WIZARA YA UJENZI:

489. MHESHIMIWA YOHANA STEPHEN MSITA (ITIGI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara kutoka Mkiwa - Mitundu - Rungwa hadi Makongorosi kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA UCHUKUZI:

490. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itakarabati Uwanja Mdogo wa Ndege (*Airstrip*) uliopo Kata ya Qurusi Wilayani Karatu.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

491. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini ujenzi wa Chuo cha Utalii katika Mji wa Njombe utaanza ili kuongeza nguvukazi katika huduma za utalii.

WIZARA YA MAJI:

492. MHESHIMIWA PROF. JOYCE LAZARO NDALICHAKO (KASULU MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa changamoto ya upatikanaji wa maji kwa Wananchi wa Muhunga na Marumba.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

493. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itajenga majosho katika maeneo ya Wafugaji ya Mahanga, Tingirima, Nyaburundu, Nyabuzume, Kiloreli na Tiring'ati.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

494. MHESHIMIWA MWINYI JAMAL RAMADHAN (BUMBWINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Wizara ya Elimu imeshawahi kukaa na Vyuo Vikuu kuwaelekeza kubadilisha Mitaala ili kuwawezesha Vijana kujiajiri baada ya kumaliza.

WIZARA YA KILIMO:

495. MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Mikataba kati ya Benki na AMCOS itatumia
Lugha ya Kiswahili.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha
Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya
Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

DODOMA
02 JUNI, 2026

BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE

